



# Dawa ya Maambukizo Fiche ya TB 3HP

Utakunywa dawa yako mara moja kwa wiki kwa wiki 12.

Utameza vidonge vyako vya kila wiki pamoja kwa wakati mmoja, siku ile ile ya wiki.

Waambie madaktari wako wengine kwamba unatumia dawa ya maambukizo fiche ya TB (LTBI).



Una maambukizo fiche ya TB, aina ya maambukizo ya TB. Huna ugonjwa wa TB na huwezi kueneza TB kwa watu wengine. Dawa hii itasaidia kuzuia ugonjwa wa TB amilifu.



Piga simu muuguzi wako ikiwa una maswali au madhara:


Dawa	Idadi ya vidonge	Siku ya wiki
Isoniazid		Jumatatu Jumanne Jumatano Alhamisi Jumamosi Jumapili
Rifapentine		Jumatatu Jumanne Jumatano Alhamisi Jumamosi Jumapili
Pyridoxine (vit B6)		Jumatatu Jumanne Jumatano Alhamisi Jumamosi Jumapili



ACHA kutumia dawa zako mara moja na UPIGIE SIMU muuguzi wako wa TB ikiwa una matatizo yoyote kati ya yafuatayo:

- Hamu kidogo au hakuna hamu ya chakula
- Kuumwa kwa tumbo au mkakamao wa misuli ya tumbo
- Kichefuchefu ama kutapika
- Mkojo wa rangi ya kola au vinyesi vyepesi
- Ngozi au macho ya manjano
- Kuchibuka au kutokwa na damu kwa urahisi
- Upele au kuwashwa
- Udhaifu mkubwa au uchovu
- Homa
- Maumivu ya kichwa ama mwili
- Kizunguzungu
- Kuwashwa au kufa ganzi katika mikono au miguu yako

**KUMBUKA: Ni sawa ikiwa mkojo, mate, au machozi yako yanageuka rangi ya chungwa. Lenzi laini za mgusano zinaweza kuwa na madoa.**



## Vidokezo vya kutumia 3HP

- Weka king'ora ili kukukumbusha kunywa dawa yako
- Mwombe mtu wa familia au rafiki ili akukumbushe
- Ongea na daktari wako ikiwa unakuywa pombe, pombe inaweza kusababisha madhara
- Mwambie daktari wako kuhusu dawa nyingine ambazo unatumia
- Mwulize muuguzi wako ikiwa una maswali